BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2018

# 03 MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2018

# 03 MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na;
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI ........................................................................ 3

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha ............................ 3

2.1.1 Swali la 1: Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii ................. 3

2.1.2 Swali la 2: Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali ........................................................................ 14

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi ........................................... 19

2.2.1 Swali la 3: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka. ......................................................... 20

2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku. ........................................................................ 28

3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI ............................. 34

4.0 HITIMISHO ........................................................................ 35

5.0 MAPENDEKEZO ........................................................................ 35

6.0 KIAMBATISHO ........................................................................ 37

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2018 kwa somo la Maarifa ya Jamii, imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu. Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne umetayarishwa kwa kuzingatia mabadiliko yaliyofanyika katika Mtaala wa Elimu ya Msingi kwa darasa la III – IV wa mwaka 2016. Upimaji huu ni wa kwanza kufanyika kwa kuzingatia mtaala huo mpya. Kwa hiyo, majibu ya wanafunzi katika upimaji yanaweza kutumika kama kiashiria kimojawapo kuhusu ufanisi wa utekelezaji wa mtaala huo mpya.

Katika taarifa hii, mambo ambayo yamechangia wanafunzi kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri, yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali umetokana na uelewa mzuri wa mahitaji ya kila swali na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Aidha, wanafunzi ambao hawakufaulu vizuri ni wale ambao wameshindwa kutambua mahitaji ya maswali kutokana na umahiri mdogo katika stadi za kusoma na kuandika. Wanafunzi wengine hawakuwa na umahiri wa kutosha katika maeneo yaliyotahiniwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri ulifanyika na kuonesha kuwa katika kila umahiri uliopimwa, wanafunzi wamefanya vizuri. Hata hivyo, nguvu zaidi katika ufundishaji wa somo la Maarifa ya Jamii inatakiwa kuwekwa katika umahiri mkuu unaohusu matumizi ya ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku. Umahiri huu ulionekana kuwa na ufaulu wa chini ikilinganishwa na umahiri mwingine katika somo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho unaotokana na ripoti hii utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia, Baraza linatarajia kuwa mamlaka husika zitahakikisha dosari zilizoainishwa katika

taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza umahiri kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuingia darasa la tano.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dr. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) uliofanyika tarehe 22 na 23 Novemba 2018, umezingatia matakwa ya mabadiliko ya muhtasari yanayolenga zaidi katika kuwawezesha wanafunzi kupata umahiri zaidi, badala ya ule wa awali ambao ulijikita katika maarifa pekee. Kwa kuzingatia matakwa hayo,upimaji huu pia ulilenga katika kupima umahiri ulioainishwa kwenye muhtasari. Hivyo, utendaji wa wanafunzi katika upimaji umegawanyika katika makundi manne yaani; **Utendaji Hafifu**, **Utendaji wa Wastani, Utendaji Mzuri na Utendaji Mzuri Sana**. Wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu katika somo la Maarifa ya Jamii walihesabika kutofaulu katika upimaji. Wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani hadi utendaji mzuri sana ndio waliofaulu katika upimaji huo.

Jumla ya wanafunzi **1,300,939** walifanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne ambapo wanafunzi **1,193,562** sawa na asilimia **91.75**, walifaulu na wanafunzi **107,260** sawa na asilimia **8.25** hawakufaulu.

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii ulikuwa na maswali 25 ambayo yaligawanywa katika sehemu kuu mbili; A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 2 ambayo ni; swali la 1 na la 2 yenye jumla ya vipengele 14 kutoka katika mahiri kuu mbili ambazo ni; *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* (ilitoka swali la 1(i) hadi (viii), *na kutumia kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishajimali* (ilitoka swali la 2(i) hadi (vi). Sehemu B ilikuwa na maswali 2 (swali la 3 na la 4) yenye jumla ya vipengele 11 kutoka katika mahiri kuu mbili ambazo ni; *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* (ilitoka katika swali la 3(i) hadi (vii), na *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku*

(ilitoka swali la 4(i) hadi (iv). Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili. Aidha, katika sehemu A, wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kwa kuoanisha maelezo ya fungu A na yale ya fungu B, kisha kuandika herufi kwenye mabano. Katika Sehemu B swali la 3, wanafunzi walitakiwa kusoma habari, na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Katika swali la 4, wanafunzi walitakiwa kusoma ramani ya kijiji cha Mtakuja kabla ya kujibu swali la 4(i) hadi (iv).

Katika taarifa hii, utangulizi utafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Wanafunzi walioweza kuonesha utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana (waliofaulu) katika kila swali watabainishwa. Aidha, wanafunzi waliobainika kuwa na utendaji hafifu (hawakufaulu) watabainishwa pia. Sababu za kila kundi kuwa na umahiri waliouonesha pia zitachambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali utafuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo itafuatiwa na hitimisho na baadaye mapendekezo yatakayotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vilizingatia asilimia ya wanafunzi waliofanya swali husika. Iwapo watahiniwa kati ya asilimia 0 hadi 33 tu ndio walioweza kujibu swali hilo kwa usahihi, kiwango hiki cha ufaulu kilihesabika kuwa ni **hafifu**. Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo kwa usahihi ni kati ya asilimia 34 hadi 66 ufaulu huo ulihesabika kuwa ni wa ***wastani,*** na kiwango cha kufaulu kilihesabika kuwa ni ***kizuri*** iwapo watahiniwa walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 hadi 100. Katika uchambuzi huu, rangi ya kijani, njano na nyekundu zilitumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu kwa mfuatano.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI

Kwa ujumla uchambuzi wa maswali unaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri katika maswali yote. Katika sehemu hii, kila swali limechambuliwa na utendaji wa wanafunzi kubainishwa. Vielelezo vimetumika kuthibitisha hoja zilizotolewa katika kila swali

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye jumla ya vipengele 14. Swali la 1 lilikuwa na vipengele nane vya maswali ya kuchagua ambapo kila mwanafunzi alitakiwa kusoma swali na kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi alizopewa. Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha ambalo lilikuwa na vipengele sita ambavyo kila mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka fungu A na kuoanisha na majibu sahihi kutoka fungu B.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii


Swali hili lilikuwa na vipengele nane; (i) hadi (viii) vilivyopima umahiri wa wanafunzi katika *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii.* Katika swali hili, wanafunzi walipaswa kusoma swali kisha kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika chaguzi zilizokuwepo katika kila swali, na kisha kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku kilichokuwa kwenye swali. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16. Katika swali hili, mwanafunzi angekuwa na *utendaji hafifu* iwapo angeshindwa kujibu kipengele hata kimojawapo, au angeweza kujibu vipengele viwili peke yake. Mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa ufasaha vipengele vitatu hadi vitano

alikuwa na *utendaji wa wastani,* na mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele sita hadi saba alikuwa na *utendaji mzuri*. Kwa upande mwingine, mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa ufasaha vipengele vyote vinane alikuwa na *utendaji mzuri sana*.

Jumla ya wanafunzi 1,300,939 (100%) walijibu swali hilo ambapo wanafunzi 31,792 (2.4%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi 211,918 (16.3%) walikuwa na utendaji mzuri, ambapo kati yao wanafunzi 139,107 (10.7%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele sita na wengine 72,811 (5.0%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele saba vya swali hilo.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 775,879 (59.7%) walikuwa na utendaji wa wastani ambapo kati yao wanafunzi 269,834 (20.7%) walipata kwa usahihi vipengele vitatu, 283,145 (21.8%) walipata vipengele vinne na wanafunzi 222,900 (17.1%) walipata vipengele vitano.

Aidha, wanafunzi 281,469 (21.6%) walikuwa na utendaji hafifu, hivyo kutofaulu swali hilo. Pia, wanafunzi 26,134 (02%) hawakuweza kujibu kabisa kwa usahihi vipengele vyote vya swali hilo na wengine 82, 384 (6.3%) waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu, wakati wanafunzi 172,952 (13.3%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele viwili. **Chati Na. 1** inaonesha mchanganuo wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 1:** kinaonesha umahiri wa wanafunzi katika kila kundi ambapo ufaulu wa jumla ni mzuri.

Uchambuzi zaidi katika majibu ya wanafunzi ulifanyika na kubaini mambo mbalimbali kama yanavyooneshwa katika kila swali kama ifuatavyo:

(i) Bwana Juma huishi na mkewe, watoto wawili na dada yake. Hii ni aina gani ya familia?

A Familia ya awali.

B Familia ya mzazi mmoja.

C Familia pana.

D Familia ya makubaliano.

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka, na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini aina ya familia inayomhusisha Bwana Juma na mkewe, watoto wawili na dada yake. Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwani, wanafunzi waliweza kuchagua jibu sahihi *C. Familia pana*. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kutosha wa kubaini kuwa, familia pana ni aina ya familia

inayohusisha baba, mama, watoto na jamaa wengine ambao wanaweza kuwa bibi, babu, kaka au hata dada wa baba au mama.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi; *A. Familia ya wa awali, B. Familia ya mzazi mmoja* na *D. Familia ya makubaliano*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulisababishwa na wanafunzi kutokuwa na umahiri wa kutosha kuhusu uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka, hasa makundi au aina za familia. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A. Familia ya awali* hawakuweza kutambua kwamba, familia ya awali ni aina ya familia ambayo inahusisha wazazi wawili na watoto wao tu, haihusishi dada wa baba. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B. Familia ya mzazi mmoja* walishindwa kubaini kuwa, familia ya mzazi mmoja ni aina ya familia inayoundwa na mzazi mmoja tu, yaani baba au mama peke yake na watoto. Familia hii hutokea pale mzazi mmoja anapofariki au kuachana kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, waliochagua Kipotoshi *D. Familia ya makubaliano* walishindwa kutambua kuwa, familia ya makubaliano ni aina ya familia inayojumuisha watoto kutoka familia nyingine kwa makubaliano.

(ii) Migogoro kati ya wakulima na wafugaji husababishwa na

A Vyama vingi vya siasa.

B Uhaba wa ardhi.

C Uhaba wa mifugo na mazao.

D Kupungua kwa wafugaji.

Swali hili limetungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa kuthamini mashujaa wetu, hasa visababishi vya migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Swali hili lilikuwa linapima uwezo wa wanafunzi kutambua kinachosababisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango

kizuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B. uhaba wa ardhi*. Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya wanafunzi unathibitisha kuwa wanafunzi hao walilielewa swali. Pia walikuwa na ujuzi wa kutosha kuwa, uhaba wa ardhi hupelekea mapambano ya kutaka kumiliki ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo hasa kwa wafugaji na kwa wakulima kupata maeneo ya kuanzisha mashamba. Hivyo mapambanao hayo hupelekea migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *A. Vyama vingi vya siasa*. Uchaguzi huu ulisababishwa na ufahamu wa kimazoea katika jamii wanayoishi ambayo imegubikwa na migogoro ya kisiasa inayochochewa na migongano katika vyama vya siasa. Pia, kipotoshi *C. Uhaba wa mifugo na mazao* kilichaguliwa na baadhi ya wanafunzi ambao walishindwa kubaini kuwa uhaba wa mifugo na mazao ni chanzo cha migogoro ya wenyewe kwa wenyewe ndani ya jamii za wafugaji au wakulima, na sio sababu ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Vilevile, wanafunzi waliochaugua kipotoshi *D. Kupungua kwa wafugaji* walishindwa kubaini kuwa, kupungua kwa wafugaji hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa kimgogoro na wakulima. Badala yake kupungua kwa wafugaji ni chanzo cha kuepuka migogoro kati ya wafugaji na wakulima kwani mapambano ya kudhibiti ardhi kati ya wakulima na wafugaji hupungua.

(iii) Dada wa baba yangu huitwa

A Mama.
B Bibi.
C Shangazi.
D Dada.

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka. Pia lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua misamiati ya majina ya watu katika familia kama yanavyotumika katika maisha ya kila siku. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni kwa kiwango kizuri, ambapo wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C. Shangazi*. Uchaguzi huu ulisababishwa na uwezo wa wanafunzi kuhawilisha ujuzi kutoka katika familia zao ambazo nyingi ni familia pana zinazohusisha baba, mama na jamaa wengine.

Hata hivyo, wanafunzi wachache walishindwa kuchagua jibu sahihi na hivyo kuchagua vipotoshi; *A. Mama, B. Bibi* na *D. Dada*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulisababishwa na wanafunzi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa misamiati ya majina ya watu katika familia, au hata kushindwa kuhawilisha kutoka katika familia zao. Wanafunzi hao hawakuweza kutambua kwamba; Mama ni mzazi wa kike, Bibi ni mzazi wa kike wa baba au mama, wakati Dada ni ndugu wa kike katika familia moja.

(iv) Kwanini tunawakumbuka viongozi wetu wakuu wa nchi ya Tanzania wa zamani?

A Walituletea amani na umoja
B Walituletea fedha za kutosha.
C Walituletea utawala wa kigeni.
D Walituletea mifarakano

Swali hili limetoka kwenye umahiri mahususi wa kuthamini mashujaa wetu, hasa kufafanua mchango wa viongozi wakuu wa serikali katika Tanzania tangu uhuru. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua mchango wa viongozi wakuu wa nchi ya Tanzania wa

zamani baada ya uhuru. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A. Walituletea amani na umoja.* Uchaguzi wa jibu sahihi unaweza kuwa umesababishwa na wanafunzi kuwa na ujuzi wa kutosha na uelewa wa kina kwamba; amani, usalama, utulivu na umoja wa watu katika nchi ni matokeo ya jitahada kubwa zilizofanywa na viongozi wetu wa zamani; na hivyo kuwa ni miongoni mwa  sababu ya kuwakumbuka viongozi wetu wakuu wa nchi ya Tanzania wa zamani.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *B. Walituletea fedha za kutosha*.  Fedha za kutosha ziliwavuta wanafunzi kuchagua kipotoshi hicho kutokana kuhusianisha nafasi ya viongozi wa taifa na uwezo wa kifedha katika kuchangia maendeleo ya taifa. Aidha, kipotoshi *C. Walituletea utawala wa kigeni* kilichaguliwa na wanafunzi ambao walihusianisha historia ya Tanzania kabla ya uhuru ambapo baadhi ya viongozi wa jadi wa jamii za Tanzania walikubali tawala za kigeni. Kwa mfano, Chifu Mangungo wa Msovero ambaye alisaini mkataba wa kilaghai na muwakilishi wa Wajerumani Karl Peters uliosababisha kutawaliwa kwa nchi yetu na wageni. Pia, kipotoshi *D. Walituletea mifarakano* kilichaguliwa na wanafunzi wachache ambao walikuwa na ufahamu wa historia ya nchi nyingine za kiafrika ambazo viongozi wao walisababisha mifarakarano ya kisiasa iliyochochewa na tofauti za kiitikadi, ukabila, na hata udini. Kwa mfano, mifarakano ya ukabila katika nchi za Rwanda na Burundi iliyopelekea mauaji ya halaiki miaka ya 1990.

(v) Ni sera gani kati ya hizi iliasisiwa na Rais wa zamani Ali Hassan Mwinyi?

A Ujamaa na Kujitegemea.

B Soko huria.

C Elimu bure kwa wote.

D Ubinafsishaji.

Swali hili limetungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa kuthamini mashujaa wetu, hasa kufafanua mchango wa viongozi wakuu wa serikali katika Tanzania tangu uhuru. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini sera iliyoasisiwa na Rais wa Tanzania wa zamani ndugu Ali Hassan Mwinyi. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi waliweza kuchagua jibu sahihi *B. Soko huria*. Uchaguzi huo umesababishwa na ujuzi wa kutosha wa wanafunzi katika kutambua na kutofautisha nyakati za viongozi wakuu na sera walizoziasisi katika vipindi vyao vya uongozi. Hii ilipelekea kuwa rahisi kwa wanafunzi kubaini sera iliyoasisiwa na Rais wa zamani wa Tanzania ndugu Ali Hassan Mwinyi ambayo ni soko huria.

Aidha, wanafunzi wengine walivutwa na kipotoshi *C. Elimu bure kwa wote*. Uchaguzi huo umesababishwa na wanafunzi kuhusianisha sera ya utawala wa sasa wa awamu ya tano ya Raisi John Pombe Magufuli ya elimu bure ambayo wanafunzi wenyewe ni wanufaika wakuu hivyo, sera hii kuwa katika fikra zao. Wanafunzi wachache walichagua kipotoshi A. *Ujamaa na kujitegemea*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki umesababishwa na ujamaa na kujitegemea ambayo ni sera maarufu iliyoasisiwa na Raisi wa Tanzania wa awamu ya kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mnamo mwaka 1967. Sera hii iliyosisitiza umoja baina ya watu na matumizi bora ya

rasilimali za nchi na kuepuka kutegemea misaada kutoka ng'ambo. Hivyo, umaarufu wa sera hiyo uliwavutia wanafunzi kuchagua kipotoshi hicho. Vilevile, kipotoshi *D. Ubinafsishaji* kilichaguliwa na wanafunzi ambao hawakuweza kutambua kwamba, sera ya ubinafsishaji iliasisiwa na Raisi wa Tanzania wa awamu ya tatu ndugu Benjamini Wiliam Mkapa. Sera hii ilijikita katika kuruhusu njia kuu za uchumi kumilikishwa watu binafsi kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji na makusanyo ya serikali. Pia, sera hii ililenga katika kuchochea maendeleo ya teknolojia, kuongezeka kwa ajira na uwekezaji.

(vi) Zifuatazo ni hasara za uhusiano mbaya wa wanafunzi shuleni, **isipokuwa**:

A Kuchukia masomo.

B Kutoweka kwa amani shuleni.

C Kutengeneza maadui shuleni.

D Kukuza mshikamano shuleni.

Swali hili limetungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka. Swali liliwataka wanafunzi kubaini faida za uhusiano mwema wa wanafunzi shuleni katika mtindo wa machaguo yaliyo taja hasara mbalimbali za uhusiano mbaya wa wanafunzi shuleni, isipokuwa chaguo moja tu ambalo ndio jibu sahihi. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwani, wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *D. Kukuza mshikamano shuleni*. Uchaguzi huu ulisababishwa na wanafunzi kuwa na ufahamu wa kutosha wa kutambua faida za uhusiano mwema ambao mara nyingi husisitizwa katika mazingira ya shuleni na walimu, hivyo kuwa rahisi kuhawilisha katika kujibu swali hilo.

Hata hivyo, wanafunzi wachache walichagua vipotoshi; *A. Kuchukia masomo, B. Kutoweka kwa amani shuleni* na *C. Kutengeneza maadui shuleni*. Wanafunzi hao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Pia, hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa kutambua na kutofautisha hasara za uhusiano mbaya wa wanafunzi shuleni. Wanafunzi hao walishindwa kubaini kuwa, kuchukia masomo, kutoweka kwa amani na kutengeneza maadui shuleni ni hasara za uhusiano mbaya wa wanafunzi shuleni.

(vii) Ni kundi lipi la jamii za Kitanzania bado linaendeleza mfumo wa ujima?

A Wandorobo, Wasandawe, na Wamakonde.

B Wamasai, Wasandawe, na Wafipa.

C Wahadzabe, Wandorobo, na Wakurya.

D Wandorobo, Wasandawe na Wahadzabe.

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka, na lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini makundi mbalimbali ya jamii za Kitanzania ambazo bado zinaendeleza mfumo wa ujima. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kwani, baadhi ya wanafunzi waliweza kuchagua jibu sahihi *D. Wandorobo,Wasandawe na Wahadzabe*. Wanafunzi hao walikuwa na ujuzi wa kutosha kwamba jamii za Wandorobo, Wasandawe na Wahadzabe ni baadhi ya jamii za Kitanzania ambazo bado zinaendeleza mfumo wa ujima.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walishindwa kubaini na kutofautisha makundi ya jamii za Kitanzania ambazo bado zinaendeleza mfumo wa ujima. Kipotoshi *A. Wandorobo, Wasandawe, na Wamakonde* kilichaguliwa na wanafunzi ambao walivutwa na umaarufu wa kabila

la Wamakonde. Kabila hili katika Tanzania ni maarufu kwa ustadi wa uchongaji vinyago na ngoma ya asili iitwayo sindimba. Kipotoshi *B. Wamasai, Wasandawe na Wafipa* kimechaguliwa na wanafunzi ambao wamevutwa na umaarufu wa historia ya kabila la Wamasai katika Tanzania ya kudumisha mila na desturi hadi sasa. Aidha, kipotoshi *C. Wahadzabe, Wandorobo na Wakurya* kimechaguliwa na wanafunzi ambao wamevutwa na jamii ya Wakurya ambayo ni jamii maarufu ya wafugaji kanda ya Ziwa Viktoria ukiondoa Wasukuma.

(viii) Moja ya faida tunayoipata kwa kucheza ngoma za utamaduni ni

A Kuendeleza utandawazi.
B Kuwaburudisha wazungu.
C Kukuza mila na desturi.
D Kudumisha lugha za kigeni.

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa kudumisha utamaduni wa Mtanzania. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua faida tunayoipata kwa kucheza ngoma za utamaduni. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri sana kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C. Kukuza mila na desturi*. Uchaguzi wa jibu sahihi umeshababishwa na uwezo wa wanafunzi wa kutambua uhusiano wa moja kwa moja kati ya ngoma za utamaduni na mila na desturi; kwani ngoma ni sehemu ya mila na desturi.


Hata hivyo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi A. *Kuendeleza utandawazi*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki ulisababishwa na umaarufu wa utandawazi ambayo ni sera inayochochewa na maendeleo ya sayansi na teknolojia hasa teknolojia ya habari na mawasiliano

(TEHAMA). Hii inapelekea kuongezeka kwa muingiliano na muunganiko wa watu katika nyanja za kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Sera hii imeifanya dunia kuwa kama kijiji kimoja. Kipotoshi *B*. *Kuwaburudisha wazungu* kimechaguliwa na wanafunzi ambao waliweza kubaini kuwa faida ya ngoma za utamaduni ni kuburudisha watu. Hata hivyo, walishindwa kubaini kuwa ngoma hizo siyo tu za kuwaburudisha wazungu kama ilivyowekwa kwenye kipotoshi, bali ni burudani kwa wanajamii wote. Aidha, kipotoshi D. *Kudumisha lugha za kigeni* kimechaguliwa na wananafunzi ambao walibaini kuwa faida ya kucheza ngoma za utamaduni ni kudumisha lugha. Kwa upande mwingine, walishindwa kutambua kwamba, lugha hizo siyo za kigeni kama ilivyowekwa kwenye kipotoshi. Lugha katika ngoma za utamaduni mara nyingi ni za kudumisha lugha za asili ya wanajamii husika.

### 2.1.2 Swali la 2: Kufuata kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali

Wanafunzi katika swali hili walielekezwa kujibu kipengele cha (i) hadi (vi) kwa kuoanisha maelezo ya fursa mbalimbali kutoka **Fungu A,** na aina husika ya fursa husika kutoka **Fungu B**. Kisha walitakiwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyopewa. **Fungu A** lilikuwa na vipengele sita vya maelezo wakati **Fungu B** lilikuwa na maneno nane ambayo yalipaswa kuoanishwa. Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu 4: *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* hasa umahiri mahsusi 4.2: *kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii*. Swali hili lilipima maarifa ya wanafunzi katika kubaini fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali kama vile: mbuga za wanyama, misitu, migodi, ardhi yenye rutuba na mvua nyingi, maeneo yenye uwanda wa nyasi na maeneo yenye mito, maziwa na bahari. Jumla ya alama kwa swali hili ni 12.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,301,113 (100%), ambapo wanafunzi 360,772 (27.7%) walipata alama zote 12 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 376,816 (29%) walipata alama 8 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine wanafunzi 322,040 (24.8%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 241,485 (18.5%) walipata alama  0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuzingatia kuwa wanafunzi 1,059,628 (81.5%)  walipata alama 4 hadi 12 kama **chati Na. 2**. inavyoonesha.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 81.5 ya wanafunzi waliweza kupata alama 4 hadi 12*

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili unaonesha kwamba wanafunzi wengi walipata alama za juu kati ya 8 hadi 12. Hali hii inaashiria kuwa  walikuwa na uelewa mkubwa wa fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo tofauti kama vile: *mbuga za wanyama; misitu; migodi; ardhi yenye rutuba na mvua nyingi, maeneo yenye uwanda wa nyasi; na maeneo yenye mito, maziwa na bahari.* Hivyo waliweza kuoanisha maeneo hayo na aina ya fursa husika kama *utalii, mbao, madini, kilimo, ufugaji na uvuvi*. **Kielelzo**

**Na 1.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vema swali hili.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Fursa zilizopo maeneo yenye mbuga za wanyama. | ( G ) | A. Kilimo<br>B. Mbao |
| (ii) Fursa zilizopo maeneo yenye misitu. | ( B ) | C. Madini |
| (iii) Fursa zilizopo maeneo yenye migodi. | ( C ) | D. Uashi |
| (iv) Fursa zilizopo maeneo yenye rutuba na mvua nyingi. | ( A ) | E. Ufundi<br>F. Ufugaji |
| (v) Fursa zilizopo maeneo yenye uwanda wa nyasi. | ( F ) | G. Utalii |
| (vi) Fursa zilizopo maeneo yenye mito, maziwa na bahari. | ( H ) | H. Uvuvi |

**Kielelezo Na. 1.1.** *Kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafuzi aliyeweza kuoanisha vizuri maelezo ya fursa mbalimbali katika* ***Fungu A*** *na aina za fursa katika Fungu* ***B*** *kwa usahihi.*

Kwa upande mwingine, katika kujibu swali hili, wanafunzi wengine walimudu kueleza baadhi tu ya fursa kwa usahihi na kukosa kuelezea fursa nyingine, hali iliyopelekea ufaulu wa wastani kwa wanafunzi hao. Aidha, wanafunzi hawa waliweza kujibu kipengele kimoja hadi vitatu kati ya sita vilivyoulizwa katika swali hili. Wanafunzi hawa walielewa baadhi ya fursa zinazopatikana katika vijiji/mtaa/kata wanamoishi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walimudu kuoanisha kwa usahihi vipengele (iv), (v) na (vi) vya Fungu A kwa herufi “A”, “F”, na “H” kutoka Fungu B. Hata hivyo walishindwa kuoanisha vipengele vilivyobaki (i), (ii) na (iii) vya Fungu A kwa herufi “B”, “C” na “D” za Fungu B. Hii inathibitisha kuwa wanfunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu fursa mbalimbali na maeneo zinapopatikana. **Kielelezo Na. 1.2** kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye ufaulu wa wastani katika swali hili.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Fursa zilizopo maeneo yenye mbuga za wanyama. | ( B ) | A. Kilimo |
| (ii) Fursa zilizopo maeneo yenye misitu. | ( C ) | B Mbao |
| (iii) Fursa zilizopo maeneo yenye migodi. | ( D ) | C. Madini |
| (iv) Fursa zilizopo maeneo yenye rutuba na mvua nyingi. | ( A ) | D. Uashi |
| (v) Fursa zilizopo maeneo yenye uwanda wa nyasi. | ( F ) | E. Ufundi |
| (vi) Fursa zilizopo maeneo yenye mito, maziwa na bahari. | ( H ) | F. Ufugaji |
| | | G. Utalii |
| | | H. Uvuvi |

**Kielelezo Na. 1.2** *Kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuoanisha baadhi ya vipengele (iv), (v) na (vi) na kushindwa kuoanisha vipengele (i), (ii) na (iii)*

Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba, kulikuwa pia na wanafunzi waliopata alama 0. Hali hii inaashiria kuwa hawakuwa na maarifa juu ya umahiri mkuu unaohusu *kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali,* hasa umahiri mahsusi unaohusu *kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii*. Wanafunzi hawa walishindwa kuoanisha maelezo na aina ya fursa mbalimbali katika swali, hali inayoashiria kuwa kwa kiasi kikubwa walikuwa wakibahatisha majibu. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi wameoanisha kipengele cha (i) cha Fungu A kwa herufi “B” *Mbao* badala ya “G” Utalii. Wanafunzi hawa walishindwa kutambua kuwa mbuga za wanyama zina utajiri wa wanyama pori wa aina mbalimbali ambao ni kivutio kikubwa cha watalii. Vilevile wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa lengo kuu la uanzishwaji wa mbuga za wanyama ni kuhifadhi wanyama pori, pamoja na maliasili mbalimbali zilizomo katika mbuga husika na si upasuaji wa mbao.

Wanafunzi wengine walioanisha kipengele cha (i) na kipotoshi “F”*Ufugaji*. Jibu hili linaashiria kuwa wanafunzi hawa wana asili ya jamii za wafugaji ambao wakati mwingine huchunga mifugo yao

ndani ya hifadhi za Taifa, jambo ambalo haliruhusiwi kisheria. Katika kipengele cha (iv), wanafunzi wengine walioanisha kipengele hiki na kipotoshi “F” *Ufugaji*, badala ya “A” *Kilimo*. Hii inaonesha wanafunzi hawa hawakuelewa kwamba maeneo yenye rutuba na mvua nyingi yanafaa zaidi kwa kilimo kwani, yanaruhusu ukuaji na ustawi mzuri wa mazao. Vilevile, wanafunzi walishindwa kubaini kuwa maeneo mengi yenye rutuba na mvua nyingi yanavutia watu wengi kwa ajili ya shughuli za kilimo, hivyo yana tabia ya kuwa na uhaba wa ardhi unaopelekea ukosefu wa maeneo ya malisho ya mifugo.

Aidha katika kipengele cha (v), baadhi ya wanafunzi walikioanisha na kipotoshi “E” *Ufund*i badala ya “F” *Ufugaji*. Jibu hili linadhihirisha kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa kwamba ufundi ni taaluma/kazi ambapo mtu huandaliwa kwa kushiriki na kufaulu mafunzo. Kwa hiyo herufi “E” ilikuwa katika Fungu B kama kipotoshi kisichoendana na maelezo yoyote ya Fungu A yanayohusu fursa mbalimbali. Kipengele cha (vi) kilioanishwa pia na kipotoshi “G” *Utalii* badala ya “H” *Ufugaji*. Hii inaonesha kwamba wanafunzi hawa walikuwa na ufahamu kuwa “Utalii” waweza pia kufanyika katika vyanzo vikuu vya maji, lakini majibu yake yalikuwa nje ya matakwa ya swali. Wanafunzi walitakiwa kubainisha fursa ya moja kwa moja inayopatikana katika maeneo yenye vyanzo vya maji kama vile mito, maziwa na bahari ambayo ni *uvuvi*. **Kielelelzo Na. 1.3** kinaonesha sampuli ya majibu ambayo si sahihi ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuoanisha maelezo ya fursa zinazopatikana katika Fungu A na aina ya fursa hizo katika Fungu B.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Fursa zilizopo maeneo yenye mbuga za wanyama. | ( C ) | A. Kilimo<br>B. Mbao |
| (ii) Fursa zilizopo maeneo yenye misitu. | ( G ) | C. Madini |
| (iii) Fursa zilizopo maeneo yenye migodi. | ( F ) | D. Uashi |
| (iv) Fursa zilizopo maeneo yenye rutuba na mvua nyingi. | ( G ) | E. Ufundi<br>F. Ufugaji |
| (v) Fursa zilizopo maeneo yenye uwanda wa nyasi. | ( D ) | G. Utalii<br>H. Uvuvi |
| (vi) Fursa zilizopo maeneo yenye mito, maziwa na bahari. | ( F ) | |

**Kielelezo Na. 1.3** *kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuoanisha maelezo ya Fungu A na Fungu B.*

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi. Katika swali la 3, mwanafunzi alitakiwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hilo lilikuwa na jumla ya vipengele saba vyenye alama mbili kila kimoja hivyo kufanya jumla ya alama 14. Katika swali la 4, mwanafunzi alitakiwa kusoma ramani aliyokuwa amepewa na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Swali hilo lilikuwa na vipengele 4. Kila kipengele kilikuwa na alama 2 hivyo kufanya kuwa na jumla ya alama 8. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu katika maswali yote mawili ulikuwa mzuri ingawa ufaulu katika swali la 4 ulikuwa chini ukilinganishwa na ufaulu katika swali la 3. Uchambuzi zaidi kwa kila swali ni kama ifuatavyo:


### 2.2.1 Swali la 3: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu 1: *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka.* Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma habari waliyopewa kuhusu hali ya hewa (Tazama Kielelezo Na. 3.1), na kisha kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi. Swali lilikuwa na vipengele saba yaani (i) hadi (vii). Kipengele cha (i) kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi juu ya maana ya “Jotoridi”. Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi kutambua namna ya kujilinda wakati wa baridi, kipengele cha (iii) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini sababu ya jotoridi kuwa juu na kipengele cha (iv) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua upimaji wa jotoridi. Aidha kipengele cha (v) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini chanzo cha joto, huku kipengele cha (vi) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini madhara ya joto kali katika mazingira, na kipengele cha (vii) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua namna ya kujilinda wakati wa joto kali. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 14. **Kielelezo Na. 2.1** kinaonesha habari iliyotumika katika swali la 3.

| |
|---|
| *Hali ya joto au baridi ya sehemu au kitu huitwa jotoridi. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa kipimajoto. Chanzo cha cha joto ni jua. Kunapokuwa na joto kali tunasema jotoridi liko juu lakini kunapokuwa na baridi tunasema joto liko chini. Kunapokuwa na baridi tunashauriwa kuvaa nguo nzito kama sweta na jaketi. Wakati wa joto kali tunavaa nguo nyepesi au nguo za pamba. Hali ya joto husababisha mito na mabwawa kukauka.* |

**Kielelezo Na. 2.1** *kinaonesha habari iliyotumika katika swali la 3.*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,301,132 (100%), ambapo wanafunzi 273,063 (21%) walipata alama zote 14 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 518,159 (39.8%) walipata alama kati ya 10 hadi 12 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine wanafunzi 274,155 (21.1%) walipata alama kati ya 6 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 235,755 (18.1%) walipata alama kati ya 0 hadi 4 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa wanafunzi 1,065,132 (81.9%) walipata kati ya alama 6 hadi 14. **Chati Na. 3** inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 3.




**Chati Na. 3** *ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 81.9 ya wanafunzi waliweza kupata alama 6 hadi 14.*

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ulibainisha kuwa ufaulu ulitofautiana sana kati ya kiwango kizuri na kiwango kizuri sana (39.8%-21%). Wanafunzi waliopata alama 14 walikuwa kwenye kiwango kizuri sana cha ufaulu, ikimaanisha kuwa waliweza kujibu vipengele vyote saba vya swali hili kwa usahihi. Wanafunzi waliopata alama kati ya 10 hadi 12 walikuwa kwenye kiwango kizuri cha ufauli kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6 kati ya vipengele saba. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama kati ya 6 hadi 8 walikuwa kwenye kiwango cha wastani cha ufaulu kwa maana kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya vipengele saba. Wanafunzi waliopata alama kati ya 0 hadi 4 walikuwa kwenye kiwango hafifu cha ufaulu, ikimanisha kuwa walishindwa kujibu kipengele chochote au waliweza kujibu kwa usahihi vipengele visivyozidi viwili kati ya vipengele saba.

Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa wanafunzi waliopata alama kati ya 10 hadi 14, walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha juu ya hali ya hewa, na hasa katika vipengele vya hali ya joto au baridi ya mahali. Hii ni pamoja na mavazi ambayo huvaliwa wakati wa baridi, hali ambayo joto huwa juu, jina la kifaa kinachotumika kupima jotoridi, kuainisha chanzo cha joto, kuainisha chanzo cha mito na mabwawa kukauka, na mwisho kutambua wakati muafaka wa kuvaa nguo nyepesi na za pamba. Katika kipengele cha (i), wanafunzi walifanikiwa kuainisha kwa ufasaha kuwa hali ya joto au baridi huitwa jotoridi. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya uwezo wa kusoma habari juu ya hali ya hewa kama ujumbe mahsusi katika habari hii. Kipengele cha (ii) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini aina za nguo zinazotakiwa kuvaliwa kipindi cha baridi.


Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kikubwa kwani wanafunzi wengi waliofanya walibainisha ulazima wa kuvaa nguo nzito kama vile sweta na jaketi. Hii inamaanisha kuwa, wanafunzi walikuwa na uelewa mzuri juu ya matakwa ya swali na hivyo kujibu kipengele hiki kwa ufasaha. Pia, kwa kuwa swali hili lilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja wa maisha ya kila siku, hivyo basi baadhi ya wanafunzi walihusianisha mavazi wanayovaa kipindi cha baridi na muktadha wa swali hili na hivyo kujibu kwa ufahasa.

Vilevile, uchambuzi unaonesha kuwa kipengele cha (iii) kiliwataka wanafunzi kutaja muktadha ambao hufanya jotoridi kuwa juu.Ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kizuri kwani wanafunzi wengi waliofanya swali hili walipata jibu sahihi kwa kuandika wakati wa joto kali au jua kali. Majibu haya ni kiashiria kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kuelewa habari ipasavyo. Katika kipengele cha (iv), wanafunzi walijengewa uwezo wa kuainisha kifaa kinachotumika kupima jotoridi. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango cha juu kwani wanafunzi waliweza kubaini kuwa kipimajoto ni kipimo kinachotumika kupima jotoridi. Majibu haya ni kiashiria kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutosha katika umahiri mahsusi wa kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku. Pia, usahihi wa majibu yao umesababishwa na uhusiano uliopo kati ya kipima joto kinachotumika kupima joto la anga na kipima joto kinachotumika zahanati kujua jotoridi la mwili wa binadamu. Kipengele cha (v) kiliwaongoza wanafunzi kubainisha chanzo cha joto kulingana na muktadha wa habari waliyoisoma. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa wa kiwango kizuri kwani wanafunzi wengi waliweza kubainisha kuwa chanzo cha joto ni jua. Jibu hili lilihusiana na uzoefu wa kawaida wa wanafunzi kuwa chanzo cha joto ni jua

ambalo daima huwaka sana wakati wa mchana katika maeneo mengi hivyo kusababisha joto.

Kipengele cha (vi) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini wakati ambao mito na mabwawa hukauka. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulibainisha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kutokana na kuandika kuwa joto ndio chanzo cha mito na mabwawa kukauka. Aidha, baadhi ya wanafunzi waliandika kuwa wakati wa jua kali au jotoridi la kiwango cha juu ndipo maji hukauka kwenye mito na mabwawa. Wanafunzi hawa waliweza kujibu kwa usahihi swali hili kwani walihusianisha ufahamu wao katika maisha ya kila siku na kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji wakati wa kiangazi katika maeneo mengi ambapo jua huwa kali. Vilevile, wanafunzi waliweza kuonesha uhusiano uliopo kati ya uwepo wa jua kali na kukauka kwa vyanzo vya maji kama vile mito na mabwawa.

Uwepo wa jua kali husabisha jotoridi kuwa juu kitendo amabacho kinapelekea maji kubadilika kutoka katika hali ya kimiminika kwenda katika hali ya gesi (mvuke). Kipengele cha (vii) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini wakati muafaka wa kuvaa nguo nyepesi na zenye asili ya pamba. Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hiki kilikuwa kizuri kwani wanafunzi walijibu kuwa ni wakati wa *joto kali.* Wanafunzi hawa waliweza kuhusianisha swali hili na maisha ya kila siku kwani wakati wa joto kali watu hupenda kuvaa nguo nyepesi na za pamba ili kupunguza athari za joto katika mwili. **Kielelezo Na. 2.2** kinaonesha mfano wa majibu mazuri ya swali la tatu ya mwanafunzi mmojawapo.



**Maswali**

(i) Hali ya joto au baridi ya mahali huitwaje?

Jotoridi.

(ii) Mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi? Sweta na Jaketi

(iii) Ni katika hali gani jotoridi huwa juu? Wakati wa Joto

(iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa Kupima joto

(v) Chanzo cha joto ni nini? Jua.


(vi) Mito na mabwawa hukauka wakati gani? Joto

(vii) Nguo nyepesi na za pamba huvaliwa wakati gani?

Wakati wa joto kali

**Kielelezo Na. 2.2** *kinaonesha sampuli wa majibu sahihi ya swali la 3 ya mwanafunzi mmojawapo.*

Uchambuzi Zaidi ulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kati ya 6 hadi 8, ikiwa ni sawa na kujibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya vipengele 7. Kufaulu huku kwa wastani kulisababishwa na ukosefu wa umakini na kukosa ujuzi wa kutosha katika kusoma habari kwa kina, jambo lililopelekea kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu vipengele vingine. Mfano, baadhi ya wanafunzi walijibu vizuri kipengele cha (i), (ii), (v) na (vi) na kukosa vipengele vilivyobaki. **Kielelezo Na. 2.3** kinaonesha mfano wa majibu ya wastani ya wanafunzi.



**Maswali**

(i) Hali ya joto au baridi ya mahali huitwaje?

jotoridi.

(ii) Mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi? Sweta na jaketi.

(iii) Ni katika hali gani jotoridi huwa juu? joto.

(iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa kipimajotoridi

(v) Chanzo cha joto ni nini? jua

(vi) Mito na mabwawa hukauka wakati gani? joto.

(vii) Nguo nyepesi na za pamba huvaliwa wakati gani?

joto


**Kielelezo 2.3** *kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata ufaulu wa wastani kwa kushindwa kujibu vizuri kipengele cha (iii), (iv) na (vii).*

Pia, uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walipata alama kati ya 0 hadi 4. Hali hii inaashiria kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali katika vipengele vingi hivyo walijibu kwa usahihi vipengele si zaidi ya viwili. Mfano katika kipengele cha (i), wanafunzi wengi waliandika *jua, kipimajoto* au *joto*. Majibu haya yalisababishwa na ukosefu wa maarifa ya kutosha juu ya hali ya hewa. Katika kipengele cha (ii) wanafunzi wengi walichanganya majibu sahihi na yasio sahihi, kama vile *nguo nzito* na *nguo nyepesi*. Wengine waliandika *nguo za pamba* na *nguo za kawaida* bila kubainisha bayana kuwa ni *nguo nzito*. Katika kipengele cha (iii) wanafunzi wengi walijibu kwa kuandika aidha*, jotoridi*, au *nguo nzito* ambazo kimsingi zinaongeza joto, lakini yote hayo sio majibu sahihi kulinga na muktadha wa habari iliyosomwa. Wanafunzi wengine waliandika chanzo cha joto ni *wakati wa mchana* ambapo joto huongezeka ukilinganisha na usiku. Majibu haya ni kiashiria kuwa wanafunzi walijibu sio kutokana na habari waliyoisoma, bali kulingana na ufahamu walionao juu ya baadhi ya vitu vinavyoongeza joto.

Kipengele cha (iv) kililenga kubaini uwezo wa wanafunzi kuelezea kifaa kinachotumika kupima jororidi. Wanafunzi wengi waliojibu swali hili waliandika kipimajoto kama jibu sahihi. Huu ni ushahidi kuwa wanafunzi wengi walikuwa na maarifa ya kutosha yaliyotokana aidha na habari waliyosoma, au walihusianisha na kipimajoto kinachotumika kupima jotoridi la mwili wa binadamu kwenye zahanati na hospitalini. Wanafunzi wengi waliojibu kipengele cha (v) waliandika *moto*, *jotoridi* au *nguo nzito* kama *sweta* na *jaketi*, majibu ambayo sio sahihi kulingana na muktadha wa swali japo ni kweli yanaongeza joto. Huu ni ushahidi kuwa wanafunzi wengi waliopata kiwango hafifu cha ufaulu hawakuelewa matakwa ya swali, badala

yake walijibu kwa kutumia ufahamu au uzoefu wa jumla walionao kuhusu maswala ya hali ya hewa.


Katika kipengele cha (vi), wanafunzi wengi walikosa kwasababu waliandika *wakati wa mchana* au *jotoridi linapokuwa juu* ndiyo sababu ya mito na mabwawa kukauka. Majibu haya kimsingi yanaelekeana na uhalisia japo sio sahihi kulingana na muktadha wa habari, kwani jibu sahihi ni *hali ya joto.* Kipengele cha (vii) kilikuwa na kiwango hafifu kabisa cha ufaulu kwani wanafunzi wengi walipata alama 0 kwa kuandika kuwa nguo nyepesi na za pamba huvaliwa kipindi cha ukame au wakati *mito* na *mabwawa* imekauka, badala ya kuandika kipindi cha *joto kali.* Majibu haya ni kiashiria kuwa wanafunzi hawakuwa makini katika kusoma habari husika, au walikosa maarifa ya kutosha juu ya maswala ya hali ya hewa. **Kielelezo Na. 2.4** kinaonesha sampuli ya majibu hafifu ya mwanafunzi katika swali la 3.


(i) Hali ya joto au baridi ya mahali huitwaje?
Joto lidi.
(ii) Mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi? Sweta.
(iii) Ni katika hali gani jotoridi huwa juu? Kiangani
(iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa Sweta
(v) Chanzo cha joto ni nini? Kipimajoto
(vi) Mito na mabwawa hukauka wakati gani? Wakati wa kiangazi
(vii) Nguo nyepesi na za pamba huvaliwa wakati gani?
Kiangazi

**Kielelezo Na. 2.4** *kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi mwenye ufaulu hafifu kwakupata vipengele viwili yaani (i) na (ii) kati ya saba vya swali la 3.*


### 2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku.

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu 3: *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku.* Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma kwa makini ramani ya kijiji cha Mtakuja waliyopewa (Tizama Kielelezo Na. 4.1), na kisha kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizo wazi. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne (i), (ii), (iii) na (iv). Kipengele cha (i) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini idadi ya madaraja yaliyopo katika ramani. Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini idadi ya milima iliyopo katika ramani, kipengele cha (iii) kililenga kupima idadi ya visima vilivyopo katika ramani. Kipengele cha mwisho (iv) kililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini hatma ya maji kutoka mto B. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 8. **Kielelezo Na. 2.5** kinaonesha ramani ya kijiji cha Mtakuja iliyotumika katika swali la 4.




**Kielelezo Na. 2.5:** *Kinaonesha ramani ya Kijiji cha Mtakuja iliyotumika katika swali la 4*.


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,301,055 (100%), ambapo wanafunzi 338,435 (26%) walipata alama zote 8 ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 382,180 (29.4%) walipata alama 6 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine wanafunzi 180,567 (13.9%) walipata alama 4 ambao ni ufaulu wa wastani na wanafunzi 399,873 (30.7%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa wanafunzi 901,182 (69.3%) walipata alama 4 hadi 8. **chati Na. 4** inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 4.




**Chati Na. 4** *ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 69.3 ya wanafunzi waliweza kupata alama 4 hadi 8*

Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na ufaulu kwenye maswali mengine katika mtihani wa Maarifa ya Jamii. Hii ni kwa sababu asilimia 30.7 ya wanafunzi walipata alama kati ya 0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kiwango hiki hafifu cha ufaulu katika swali hili ni kikubwa ikilinganishwa na viwango hafifu vya ufaulu katika swali la 1, 2, na la 3 ambavyo ni 21.6%, 18.5% na 18.1% mtawalia. **chati Na. 5** inaonesha kiwango

cha ufaulu kwa swali la 4 ikilinganishwa na maswali mengine katika mtihani wa Maarifa ya Jamii.





**Chati Na. 5** *kinaonesha kiwango cha ufaulu kwa swali la 4 ikilinganishwa na maswali mengine katika mtihani wa Maarifa ya Jamii.*

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ulibainisha kuwa, ufaulu ulitofautiana sana kati ya kiwango cha wastani na kiwango hafifu (13.9%-30.7%). Wanafunzi waliopata alama 8 waliweza kujibu vipengele vyote vinne vya swali hili kwa usahihi. Wanafunzi waliopata alama 6 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 kati ya vipengele 4. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 4 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 2 kati ya vipengele vinne, na wanafunzi waliopata alama 0 hadi 2 aidha hawakuweza kujibu kwa usahihi kipengele chochote au waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja kati ya vipengele vinne.

Kwa ujumla, swali hili lililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika nyanja kuu mbili; kwanza lilipima uwezo wa wanafunzi kusoma na kutafsiri ramani, na pili lilipima uwezo wa kuhesabu idadi ya vitu mbalimbali vilivyooneshwa katika ramani. Wanafunzi waliopata alama 6 hadi 8 walikuwa na umahiri wa kutosha katika kutumia

ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku. Kufaulu huku kunaashiria kuwa wanafunzi hawa walijibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4, yaani kubaini idadi ya madaraja, milima, visima na hatima ya maji ya mto B. Katika kipengele cha (i), wanafunzi waliojibu kwa usahihi waliweza kubaini madaraja mawili yaliyopo katika ramani. Uwezo huo ulitokana na maarifa ya kutosha juu ya usomaji wa ramani waliyonayo wanafunzi. Katika kipengele cha (ii), wanafunzi walioweza kujibu kwa usahihi walibaini milima mitatu iliyopo katika ramani. Katika kipengele cha (iii), wanafunzi waliojibu kwa usahihi waliweza kubaini uwepo wa kisima kimoja, na kipengele cha mwisho (iv) wanafunzi walifanikiwa kubaini kuwa mto B unamwaga maji yake katika bwawa. Aidha wanafunzi wengi waliopata alama 6 walikosa katika kipengele cha (iv) kwani wengi wao waliandika *msitu* na wengine *kusini.* Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo mzima wa mto kutoka kwenye chanzo hadi unapoishia ambapo inaweza kuwa chanzo cha maji kama vile bwawa, ziwa au bahari. **Kielelezo Na. 2.6** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu vizuri swali la 4.


(i) Kuna madaraja mangapi katika ramani?
Mawili.
(ii) Kuna milima mingapi katika ramani?
Mitatu.
(iii) Kuna visima vingapi katika ramani?
Kimoja.
(iv) Mto B unamwaga wapi maji yake?
Bwawa.

**Kielelezo Na. 2.6** *kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vizuri vipengele vinne vya swali la 4*

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4 ikiwa ni sawa na kujibu kwa usahihi vipengele 2 kati ya 4. Kufaulu huku kunatokana na wanafunzi kuwa na uwezo mzuri wa kusoma ramani, lakini kukosa uwezo wa maarifa juu ya kuhesabu ili kujua idadi vitu mbalimbali katika ramani na kinyume chake. Kwa mfano kipengele cha (iii) na (iv) ni miongoni mwa vipengele ambavyo wanafunzi wengi walifanya vibaya. Kipengele cha (iii) wanafunzi wengi waliandika kuna visima viwili katika ramani na wakati kwa uhalisia kuna kisima kimoja. Wanafunzi hawa walichanganya na majosho kutokana na kukosa maarifa ya kusoma ramani.

Kulikuwa na majibu mbalimbali ambayo wanafunzi waliandika katika kipengele cha (iv). Baadhi ya wanafunzi waliandika mto B unamwaga maye yake *milimani,* wengine *msituni*, na wachache waliandika *shuleni* na *kusini*. Kimsingi mlimani ni sehemu ambayo mto B umeanzia; msitu na shuleni vipo sambamba na bwawa sehemu ambayo mto B unaishia. Hivyo basi, wanafunzi hawa walishindwa kutambua ni wapi mto unamwaga maji na kuandika mlimani, shuleni na msituni majibu ambayo si sahihi. Hii inaashiria kuwa mbali na ujuzi wa kusoma ramani wanafunzi hawa hawakuwa ujuzi juu ya mfumo mzima wa mto kutoka kenye chanzo hadi unapoishia. **Kielelezo Na. 2.7** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioefaulu kwa kiwango cha wastani kwa jibu kwa usahihi vipengele viwili kati ya vinne.

(i) Kuna madaraja mangapi katika ramani?

mawili

(ii) Kuna milima mingapi katika ramani?

miwili

(iii) Kuna visima vingapi katika ramani?

kimoja

(iv) Mto B unamwaga wapi maji yake?


Zaidi kushinda maji

**Kielelezo Na. 2.7** *kinaonesha mfano wa majibu ya mwanafunzi mwenye ufaulu wa wastani aliyepata vipengele viwili yaani (i) na (iii) kati ya saba vya swali la 4.*

Pia uchambuzi unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi walipata alama kati ya 0 hadi 2, hali inayoashiria uwezo mdogo kabisa waliokuwanao katika kujibu vipengele vyote vinne. Wanafunzi wengi katika kundi hili walifanikiwa kujibu kipengele kimoja kati ya vipengele vinne, na wengine hawakujibu kabisa kipengele chochote. Kipengele cha (i) kilionesha kujibiwa vizuri na wanafunzi wengi ikiwemo wanafunzi wenye ufaulu hafifu, kwani waliweza kutaja idadi ya madaraja yaliyowakilishwa katika ramani ambayo ni mawili. Ufaulu mzuri katika kipengele hiki (i) ulichangiwa na alama iliyotumika kuwakilisha daraja kwani ni alama inayofahamika miongoni mwa wanafunzi wengi. Alama hiyo inatumika kama moja ya alama za barabarani kuonyesha daraja. Vilevile, kipengele hiki (i) kilijibiwa vizuri na wanafunzi wengi kutokana na jinsi alama hizo za madaraja zilivyowakilishwa katika ramani kwani zilikuwa zinaonekana kwa urahisi sehemu ambapo mito A na B ilipokatisha barabara.

Vipengele vingine (ii), (iii) and (iv) vilijibiwa vibaya na wanafunzi wengi hasa walio katika kundi hili la ufaulu hafifu. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na ufahamu na maarifa ya kutosha juu usomaji na utafsiri wa ramani, hivyo walishindwa kutoa majibu sahihi kwa vipengele vitatu vya swali husika. Baadhi ya

wanafunzi katika kundi hili la ufaulu waliandika maswali kama yalivyoulizwa bila kutoa majibu, huku wengine wakiandika manemo yaliyoulizwa katika maswali kama vile milima, madaraja na visima bila kutoa majibu sahihi. Wanafunzi wengine waliandika majina ya vitu vilivyoorodheshwa katika ufunguo wa ramani bila kuzingatia matakwa ya swali. **Kielelezo Na. 2.8** kinaonesha mfano wa majibu ambayo si sahihi kama alivyojibu mwanafunzi mmojawapo.



(i) Kuna madaraja mangapi katika ramani?

madaraja matatu.

(ii) Kuna milima mingapi katika ramani?

4.

(iii) Kuna visima vingapi katika ramani?

2.

(iv) Mto B unamwaga wapi maji yake?

3.

**Kielelezo Na. 2.8***. Sampuli ya majibu ya wanafunzi alioshindwa kutafsiri ufunguo na hivyo kushindwa kujibu swali kwa usahihi***.**

## 3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI

Uchambuzi katika mtihani wa Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2018 unaonesha kuwa, kati ya mahiri kuu nne zilizopimwa kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016 ulikuwa na ufaulu mzuri katika mahiri zote nne. Hata hivyo, ufaulu katika moja ya umahiri (matumizi ya ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku) ulikuwa chini (69.3%), ikilinganishwa na mahiri nyingine tatu. Kwa mfano, ufaulu wa wanafunzi katika umahiri wa kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka ulikuwa asilimia 81.9, wakati ambapo ufaulu katika umahiri katika kufuata kanuni za kiuchumi katika uzalishaji mali ulikuwa asilimia 81.5. Kwa upande mwingine, umahiri katika kutambua misingi ya uzalendo katika jamii ulikuwa

asilimia 78.4. Kwa hiyo, inaweza kuhitimishwa kuwa, ingawa wanafunzi wameweza kupata umahiri unaokubalika katika mahiri zote nne kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari, bado wanafunzi wanaupungufu wa umahiri, hasa kwenye stadi za kusoma ramani. Inaweza kuzingatiwa pia kuwa, nguvu inatakiwa kuwekwa katika kuwasaidia wanafunzi kupata umahiri unaokubalika katika kutambua misingi ya uzalendo katika jamii wakati wa mchakato wa kujifunza na kufundisha. Jedwali Na. 1 linaonesha mchanganuo wa ufaulu katika kila umahiri kwa kifupi.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa darasa la nne katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha ufaulu wa mahiri zote katika kiwango kizuri. Aidha, kulikuwa na changamoto za kushindwa kuelewa uhitaji wa swali, ujuzi hafifu katika umahiri mahususi na kushindwa kuhawilisha ujuzi kutoka katika jamii. Hata hivyo, wanafunzi wengi wameweza kuonesha umahiri wa kutosha uliyowawezesha kubaini majibu sahihi katika maswali yaliyoulizwa na hivyo kuwa na utendaji mzuri (kufaulu).

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha utendaji wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wasisitizwe kupima umahiri wa wanafunzi katika stadi za kusoma na kuandika ili kuweza kuwasaidia wanafunzi walio na ujuzi mdogo wa kusoma na kuandika.

(b) Baadhi ya wanafunzi walionesha udhaifu katika ujuzi wa ufahamu. Mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji

zitumike katika masomo yanayolenga kukuza ujuzi wa ufahamu wa wanafunzi.

(c) Mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zitumike katika umahiri wa kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku ili kukuza ujuzi wa wanafunzi hasa katika kutumia vipengele muhumu vya ramani kama vile ufunguo. Kipengele hiki kilionekana kutoeleweka vizuri kwa wanafunzi wengi waliofanya mtihani wa darasa la nnne (SFNA) kwa mwaka 2018.

(d) Wanafunzi wasisitizwe kusoma kwa umakini vitabu vya kiada na ziada ili kujiongezea ujuzi na uwezo wa kujibu maswali kwa usahihi.

(e) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha yanayolenga kukuza umahiri ili kuwajengea uwezo katika kujibu maswali yanayopima umahiri.

(f) Mamlaka husika zifuatilie na kusimamia kwa umakini mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kubaini changamoto zinazozuia ujifunzaji na ufundishaji kuwa na ufanisi na kuziondoa ikiwezekana.

## 6.0 KIAMBATISHO

**Jedwali Na 1:**

**KUFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2018**

| Na | Umahiri | Ufaulu kwa kila swali | |
|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | % ya kufaulu |
| 1. | Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka mwanafunzi | 3 | 81.9 |
| 2. | Kutumia kanuni za kiuchumi katika uzalishaji mali | 2 | 81.5 |
| 3. | Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii | 1 | 78.4 |
| 4. | Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | 4 | 69.3 |